The Project is funded by the European Union

# KIJARIDA CHA MRADI WA KUONGEZA THAMANI KATIKA MISITU YA MILIMA YA TAO LA MASHARIKI (AVA)

*Kimechapishwa Machi 2016*

## AVA NINI?

AVA ni mradi wa kuongeza thamani katika Misitu ya Tao la Mashariki (Adding Value to the Arc)

Mradi unafadhiliwa na Umoja wa nchi za Ulaya kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2013 hadi 2017.

Lengo ni kupunguza umasikini na kuboresha shughuli za kiuchumi kwa jamii zinazoishi kando kando ya misitu zinazotegemea rasilimali zinazotokana na misitu iliyoko wilaya ya Mvomero.

Mradi unatekelezwa kwenye vijiji 34 vilivyo kando kando ya Msitu wa Hifadhi wa Kanga (Bwage, Mziha, Difinga, Kibatula Kanga na Dihinda) na Hifadhi ya Mazingira Asilia ya Mkingu (Mhonda, Kwelikwiji, Mafuta, Ubiri, Mlaguzi, Komtonga, Mbogo, Kigugu, Kwadoli, Digoma, Digalama,Msolokelo, Pemba, Gonja, Makate, Kinda, Semwali, Maskati, Dibago,Hembeti, Mkindo, Mndela, Kisimaguru, Msufini, Dihombo na Makuyu. Vijini vingine vinne ambavyo havijagusa hifadhi hizi lakini vina misitu mizuri ya jamii ni Masimba, Ndole, Magunga na Diburuma. Kwa ujumla misitu hii ni chanzo muhimu cha maji na sehemu ambapo kuna wanyama na mimea ya kipekee.

### MATARAJIO YA MRADI

1. Usimamizi shirikishi wa misitu kwa jamii.
2. Usimamizi shirikishi wa misitu kwa pamoja.
3. Kuibua miradi rafiki na mazingira kwa ajili ya kuongeza kipato kwa wanajamii.
4. Kujenga uwezo na kuimarisha utawala bora.
5. Ufuatiliaji na upashanaji wa habari

## MRADI UMEFANYA NINI KWA KIPINDI CHA MWAKA 2015

### USIMAMIZI SHIRIKISHI WA MISITU KWA JAMII

- Kutambulisha na kujenga uelewa juu ya mradi kwenye vijiji vya Usimamizi Shirikishi wa misitu Kwa jamii
- Kuwezesha jamii kuanzisha na kusimamia misitu ya kijiji
- Kupitishwa kwa Mipango ya Usimamizi shirikishi kwa jamii katika ngazi ya kijiji na wilaya
- Mipango ya Matumizi Bora ya ardhi
- Mafunzo kwa kamati za maliasii za vijiji, kamati za matumizi bora ya ardhi na viongozi wa serikali za vijiji

### USIMAMIZI SHIRIKISHI WA MISITU KWA PAMOJA

- Mafunzo ya kamati za maliasili, viongozi wa serikali ya kijiji na halmashauri ya kijiji juu ya Usimamizi wa Misitu kwa Pamoja
- Kununua na Kusambaza vitendea kazi kwa ajili ya Kamati za maliasili kwenye vijiji vinavyoshiriki kwenye usimamizi shirikishi wa Misitu kwa pamoja
- Kusambaza vifaa vya kuendeshea ofisi (Shajala)

*Wanawake nao wana haki ya kumiliki ardhi sawa na wanaume*

MIRADI RAFIKI NA MAZINGIRA KWA AJILI YA KUONGEZA KIPATO KWA JAMII

- Kuboresha na kuwezesha vikundi vya ukusanyaji na uuzaji wa sambu
- Kuimarisha vikundi vya Hisa
- Kuendeleza kilimo kwa kutumia mbinu za kilimo hifadhi
- kuanzisha na kuendeleza bustani za miti

KUJENGA UWEZO KWA AJILI YA KUIMARISHA UTAWALA BORA

- Mafunzo ya elimu ya mazingira kwa walimu wa shule za msingi
- Elimu ya utawala bora kwa viongozi wa serikali za vijiji, kamati za maliasili na matumizi bora ya ardhi za vijiji

UFUATILIAJI NA UPASHANAJI HABARI

- Tathmini na Ufuatliaji wa shughuli za mradi
- Mafanikio na changamoto za mradi zimechapishwa kwenye magazeti na kurushwa kwenye TV
- Uhamasishaji kupitia sinema na vijarida mbalimbali
- Warsha ya Tathmini na kupanga mpango kazi wa mwaka 2016
- Taarifa za watu waliofanikiwa katika shughuli za mradi zimeandaliwa na kurushwa kwenye vyombo vya habari

## USIMAMIZI SHIRIKISHI WA MISITU KWA JAMII (USMJ)

Ili lengo la mradi la kusaidia vijiji kutekeleza mpango wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu kwa Jamii litimie, Mradi unaendelea kupanua elimu na kusaidia vijiji vingine 2 (Ndole na Magunga) kuanzisha misitu ya Hifadhi ya Kijiji na pia kijiji kingine cha Diburuma kilipata elimu na uamasishwaji wa usimamizi wa misitu ya jamii.

*Sheria ya msitu ya mwaka 2002 inatoa fursa nyingi kwa jamii kusimamia na kulinda misitu*

*Sheria inasema kuwa miongoni mwa malengo yake makuu ni kuwapa wajibu na haki ya kusimamia misitu wananchi ndani na kandokando ya misitu*

Wanajamii walielimishwa kwamba wakiweza kutunza misitu yao watapata motisha kama:

- Kubaki na 100% ya mapato yatokanayo na mauzo ya mazao ya misitu.
- Kubaki na tozo na faini. Faini inayotozwa katika ardhi ya kijiji kutokana na Misitu ya Hifadhi ya Kijiji au Misitu ya jamii inabaki kijijini ili mradi imeelezwa kwenye sheria ndogo za kijiji.
- Utaifishaji wa mazao ya misitu na vifaa kutokana na uvunaji haramu.
- Wanaweza kufanya uvunaji endelevu wa mazao ya misitu ili mradi imeelezewa kwenye mpango wa uvunaji wa kijiji

Baada ya kuelimishwa wanavijiji wa vijiji vya Ndole, Diburuma na Magunga walianza mchakato wa kusimamia Misitu ya Hifadhi ya Vijiji. Vijiji vyote vitatu viliunda kamati ya maliasili ya kijiji yenye wajumbe 12 ikijumuisha wanaume na wanawake. Vijiji vya Magunga na Ndole walifanikiwa kutenga maeneo ya Misitu. Ndole hekta 1,238.81 na Magunga hekta 1,277.3, pia waliandaa mpango wa usimamizi wa misitu, sheria ndogo na kuidhinishwa na Mkutano mkuu wa kijiji na kupelekwa kwenye Halmashauri ya Wilaya kwa idhini na kwaajili ya kusajiliwa kwenye daftari la usajili wa misitu ya vijiji.

Hii inapelekea kufanya jumla ya hekta 10,131.22 kwa vijiji 8 (Bwage, Mziha, Difinga, Msolokelo, Masimba, Makuyu Magunga na Ndole) ambavyo vinatekeleza Usimamizi Shirikishi wa Misitu kwa Jamii na kuidhinishwa na mkutano mkuu wa kijiji. Kwa kipindi cha mwaka 2015 mpango wa usimamizi wa misitu na sheria ndogo za vijiji 3 (Makuyu, Msolokelo na Masimba) zimeidhinishwa na Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero na kusajiliwa kwenye daftari la usajili wa misitu ya vijiji.



Mpaka sasa vijiji ambavyo vinatekeleza usimamizi shirikikishi wa misitu kwa jamii ambayo imeidhinishwa na Kusajiliwa kwenye daftari la misitu ya vijiji na Kutamkwa kuwa "Msitu wa Hifadhi wa Kijiji" ni 6 (Difinga, Bwage, Mziha, Makuyu, Masimba na Msolokelo).

## MPANGO WA MATUMIZI BORA YA ARDHI

Kwa kuelewa msingi endelevu wa rasilimali za kijiji hauwezi kuwepo bila kijiji husika kuwa na mpangilio wa rasilimali zake. Mradi wa AVA umeendelea kusaidia vijiji kuandaa Mipango Shirikishi ya Matumizi Bora ya Ardhi kwenye vijiji ambavyo vinatekeleza Usimamizi Shirikishi wa Misitu Kwa jamii. Kwa kipindi cha mwaka 2015 vijiji 2 (Ndole na Magunga) vimefanikiwa kutengeneza Mpango Shirikishi wa Matumizi Bora ya Ardhi. Mipango hii imeidhinishwa na Mikutano Mikuu ya vijiji na kupelekwa Wilayani kwaajili ya kuidhinishwa na Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero. Mipango hii ya vijiji imepelekea mpaka sasa kuwa na vijiji 6 (Magunga, Ndole, Makuyu, Difinga, Bwage, Mziha ambavyo vimesaidiwa na mradi kukamilisha zoezi la Mpango Shirikishi wa Matumizi Bora ya Ardhi.

Kwa kuwapa motisha wanajamii mradi wa AVA uliwapatia hati za kimila za kumiliki ardhi wanavijiji 88. Kijiji cha Ndole wanakijiji 45 kati yao wanawake 13 na wanaume 32. Kijiji cha Magunga 43 kati yao wanawake 8 na wanaume 35.. Hililililikuwa ni zoezi la mfano ili wanajamii wengine waweze kufanya kama hawa wengine ili kila mmoja awe na hati yake ya kimila.

## USIMAMIZI SHIRIKISHI WA MISITU KWA PAMOJA

Kamati za maliasili, viongozi wa serikali za vijiji na wajumbe wa Halmashauri za vijiji kutoka vijiji 23 vinavyotekeleza Usimamizi Shirikishi wa Misitu kwa Pamoja walifundishwa juu ya miongozo ya Usimamizi Shirikishi kwa Pamoja; mfano mgawanyo wa mapato na gharama za usimamizi, makubaliano ya usimamizi na mgawanyo wa mapato kwa asilimia. Pia walifundishwa juu ya utawala bora. Mambo ya





msingi yaliyosisitizwa juu ya misingi ya utawala bora ambayo ni:

- Uwajibikaji na Uwazi
- Usawa
- Ufanisi na Tija
- Ushirikishwaji
- Mwitikio
- Maridhiano
- Uadilifu
- Utawala wa sheria

## MIRADI RAFIKI NA MAZINGIRA KWA AJILI YA KUONGEZA KIPATO KWA JAMII

### Vikundi vya hisa

Jumla ya vikundi 158 vyenye wanachama 3,790 (wanawake 2,240 na wanaume 1,550) vimeendelea kuweka na kukopa fedha kwa ajili ya maendeleo na mahitaji mengine muhimu. Kwa kipindi cha 2015 wanachama walipewa mafunzo ya mpango wa hisa. Kutokana na utafiti uliofanyika unaonesha



kwamba vikundi hivi vipo hai na vingi kati yao (90%) vinakutana mara moja kwa wiki na baadhi (10%) vinakuatana mara mbili kwa mwezi. Taarifa zinaonesha 97% ya wanachama wamefanikiwa kuchukua mikopo na wamewekeza kwenye masuala ya kilimo, ujenzi wa nyumba, biashara ndogo ndogo na ufugaji wa kuku na mbuzi. Hii ni dalili njema kuonesha uhai wa vikundi na vinasaidia kwenye maendeleo ya wanachama hasa wakina mama ambao wengi wao (59%) ni wanachama. Hii inadhibitishwa na ufuatliaji uliofanywa kati ya wanawake 100 waliohojiwa 52% waliwekeza hela zao kwenye biashara ndogo ndogo, 25% kwenye kilimo, 7% ununuzi wa vifaa vya ujenzi, kuboresha makazi na kujenga nyumba, 7% kulipa ada na matumizi mengine ya shule, 5% kulipia gharama za afya, 3% gharama za mazishi na 1% gharama za chakula na nguo.



Kabla ya kujiunga na Kikundi cha Hisa



Baada ya kujiunga na Kikundi cha Hisa

### Kilimo Hifadhi

Kwa kutambua umuhimu wa kilimo katika maeneo ya mradi katika kuinua uchumi wa wanajamii, mradi uliwapa elimu ya kilimo kupitia njia ya vikundi wanakijiji wa vijiji 7 (Masimba, Msolokelo, Difinga, Dihinda, Bwage, Kanga na Mziha). Jumla ya vikundi 20 viliundwa vikiwa na jumla ya wanachama 432 (wanawake 160 na wanaume 272). Vikundi hivi vilisaidiwa zana na pembejeo za kilimo. Pembejeo zilijumuisha mbolea aina ya DAP mifuko 20, Urea mifuko 20, mbegu aina ya STAHA kilo 20, TAN 254 kilo 160, ufuta kilo 20, Maharage kilo 160, fiwi kilo 20, mabomba ya kupulizia dawa bomba 20, lita 8 za dawa ya kuuwa wadudu na lita 20 za dawa za kuulia magugu.

Moja ya shamba darasa la Mahindi





Shamba darasa la ufuta



## UTAFITI WA KILIMO HIFADHI

Lengo la mradi ni kuboresha hali za maisha ya wanajamii wanaozunguka misitu ya Nguru kusini. Miongoni mwa shughuli za kiuchumi ni suala la kilimo, hata hivyo kilimo katika vijiji vya Nguru kusini kinakabiliwa na upungufu wa rutuba ya udongo, ufyekaji na uharibifu wa misitu hivyo kupelekea wakulima kuongeza shughuli za kilimo na uzalishaji kwa kuongeza kufyeka misitu. Kwa kuona hilo mradi ulifanya utafiti kwa kutumia mtaalam elekezi kwa masuala ya kilimo hifadhi. Utafiti huo ulitoa matokeo yafuatayo:

- Ustawi wa mazao unatofautiana maeneo ndani ya kijiji na pia kati ya kijiji. Mfano kijiji kimoja unakuta zao linastawi ukanda mmoja na ukanda mwingine wa kijiji kunastawi zao lingine. Kijiji kingine ni ukanda mmoja tu.
- **Mahindi:** Mahindi yanastawi kwenye ukanda wa chini wenye unyevu na ukanda wa juu wenye unyevu kiasi.
- **Mpunga:** Unastawi katika ukanda wa chini wenye unyevu na sehemu ya mabonde kwenye ukanda wa chini.
- **Maharage na mbaazi:** Yanastawi ukanda wa chini mkavu na ukanda wa juu wenye unyevu kiasi.
- **Migomba:** inastawi ukanda wa chini wenye unyevu kiasi na ukanda wa wa juu wenye unyevu.
- **Maparachichi:** Yanastawi sana kwenye maeneo ya ukanda wa chini wenye unyevu na ukanda wa juu wenye unyevu.
- **Cocoa:** Inastawi maeneo ya chini ya milima na maeneo ya ukanda wa chini wenye unyevu kiasi.
- **Mitiki:** Miti hii inastawi kwenye maeneo ya ukanda wa chini wenye unyevu, unyevu kiasi na baadhi ya maeneo makavu. Pia inastawi kwenye ukanda wa juu wenye unyevu kiasi.
- **Mihogo:** Inastawi vizuri kwenye maeneo ya chini ya milima na maeneo yenye unyevu kiasi kwenye ukanda wa juu na maeneo mengine yote isipokuwa kwenye mabonde yenye unyevu.
- **Nyanya:** Zinastawi vizuri kwenye maeneo makavu na yenye unyevu kwenye ukanda wa chini na yenye unyevu kiasi kwenye ukanda wa juu.
- **Ufuta na Alizeti:** Yanastawi vizuri kwenye maeneo makavu na yenye unyevu kwa ukanda wa chini na wenye unyevu wa kiasi chini ya milima.

***Gravelia na Iliki:*** Yanastawi vizuri sana kwenye mabonde makavu ukanda wa chini, chini ya milima, ukanda wa chini na wa juu wenye unyevu.


### Changamoto za soko

Utafiti huu uliona kuna changamoto kubwa ya ukosefu wa soko la uhakika wa mazao, changamoto hii inasababishwa na;

- Wafanyabiashara kutumia fursa ya wakulima kutojua bei iliyopo sokoni kwahiyo wafanyabiashara wanatumia mwanya huo kuwarubuni na kuwakandamiza wakulima.
- Maeneo mengi hayafikiki kwa usafiri wa gari na yale ambayo yanafikika barabara zake ni mbovu kwahiyo, wafanyabiashara wanatumia kama kigezo cha kununua mazao kwa bei ya chini.
- Umbali mrefu kufikia soko lilipo.
- Ushirikiano mdogo baina ya wakulima. Wakulima wangeweza kushirikiana na kupanga bei za mazao ikawa moja bila kila mkulima kuwa na bei yake mwenyewe kwa zao moja.

### Mapendekezo ya utafiti

- Njia sahihi za kuhifadhi udongo na maji zinatakiwa zitumike. Njia hizo ni kama kilimo cha kontua, fanya juu fanya chini na kilimo cha kuotesha mazao ambao yanakinga mmomonyoko wa udongo hasa kwenye



maeneo ya miinuko. Mradi unaweza kutumia uzoefu wa maeneo ya milima ya Uluguru ili kuweza kueneza utaalamu huu kwa wanakijiji wa milima ya Nguru kusini.

- ❖ Inashauriwa kukuza na kuboresha uzalishaji wa kuku wa kienyeji kama njia moja wapo ya kuwasaidia wakulima kuongeza kipato ili wajikwamuwe kwenye umasikini na wanaweza kupata kipato na wakawekeza kwenye kilimo hifadhi kinachokabiliana na mabadiliko ya tabianchi.
- ❖ Mpango wa Hisa ni mfumo ambao unafanya vizuri kwenye vijiji vya mradi. Kwahiyo kama utaendelezwa utasaidia wanajamii wengi kupata kipato na kuwekeza kwenye kilimo hifadhi ambacho kitawasaidia wanajamii kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.
- ❖ Imeshauriwa pia miti aina ya Gravelia na Mitiki inaweza kupandwa yenyewe kwenye shamba kama shamba la miti kwa wakulima wenye mashamba makubwa ya kutosha (ekari 10 au zaidi) na kwa wale wenye mashamba ya ukubwa wa kati (ekari 3 hadi 5) wanaweza kuchanganya na mazao mengine. Wakulima wenye mashamba madogo chini ya ekari 3 wapande kwenye mipaka ya mashamba yao.
- ❖ Mfumo sahihi wa kilimo mseto (kuchanganya miti na mazao ya kawaida) ambao unaunganisha kuchanganya mazao ya miti na mazao ya msimu kwa kipindi cha miaka mitano ya mwanzo ambayo itasaidia kurutubisha udongo kwa ajili ya kuzalisha mazao kama magimbi na iliki na baada ya miaka kumi miti hii inaweza kukatwa na kuacha visiki ili iweze kuchipua tena kwa mzunguko wa pili wa kilimo mseto.

Baada ya utafiti huu mradi ulitumia mapendekezo haya na kuweza kubainisha wakulima 280 kutoka kwenye vijiji 7 (Digalama, Mafuta, Kisimaguru, Dibago, Kinda, Diburuma na Pemba). Kila kijiji kimetoa wakulima 40 ambapo kila mkulima atakuwa na shamba lake na ataelekezwa mbinu za kilimo hifadhi na kupewa baadhi ya pembejeo kama sehemu ya mafunzo. Lengo la kufanya hivi ni kuwa na mashamba mengi ndani ya kijiji ambapo wanakijiji wengi wanaweza kujifunza kupitia mashamba hayo kwa kuwa wakulima hawa walichaguliwa kupitia kwenye vitongoji kwahiyo kila kitongoji kimekuwa na wawakilishi sawa.

Pia kwa kutumia ushauri wa utafiti wa kutumia mbinu zilizotumika katika milima ya Uluguru, wakulima hawa walichaguliwa baadhi ya wawakilishi (3 kutoka kila kijiji) kwa ajili ya safari ya mafunzo katika kijiji cha Kinole kilichopo tarafa ya Makuyuni, Wilaya ya Morogoro vijijini. Safari hii ambayo imefanyika Januari 2016 imejumuisha na wataalamu wa kilimo wa ngazi ya kijiji na kata.



## Vikundi vya Sambu

Mradi umeanza kufanya kazi kwenye vikundi vya kukusanya na kuuza sambu. Mpaka sasa mradi umeainisha vikundi 12 vyenye wanachama 240 kutoka kwenye vijiji 8 ambavyo ni Kigugu (1), Mafuta (2), Kwelikwiji (2),Luhamba I Ubiri (2, Digalama (2), Kinda (1) na Gonja (1). Mafunzo



ya kuboresha ukusanyaji, ukaushaji, uhifadhi na usafirishaji yalitolewa kwa wanachama wote.
Afisa miradi alikutana na kampuni inayojihusha na ununuzi wa sambu na kukubaliana kwamba kampuni itaanzisha vituo vya ukusanyaji katika vijiji vinavyofikika kwa usafiri wa gari.

Pia mradi ulitoa magunia 240 na maturubai 48 kwa wanavikundi kama njia moja wapo ya kuonyesha mfano wa sehemu bora ya kukaushia na kuhifadhi mbegu za sambu.

### BUSTANI ZA MITI

Vikundi 15 vimepewa elimu jinsi ya kuandaa vitalu vya miti. Vikundi hivi vimewezeshwa kwa kupewa vitendea kazi; chepe 30, Viriba kilo 30, reki 15, keni 30 za umwagiliaji na mipira 15 ya umwagiliaji. Pia walipatiwa aina mbalimbali ya mbegu zinazoendana na mazingira ya eneo lao. Mradi ulitoa mbegu kilo 2 za Gravelia, kilo 1 ya *Gliricidia sepium seeds* na kilo1 ya *Albizia versicolar.*



### UFUATILIAJI NA UPASHANAJI HABARI

Kwa kutambua umuhimu wa kufuatilia shughuli za mradi na kupashana taarifa. Mradi umefuatilia utendaji wa kamati za maliasili, vikundi vya Hisa na hali ya uharibifu kwenye misitu ya Mkingu. Jumla ya doria 355 ndani ya mwaka 2015 zimefanywa na kamati za maliasili za vijiji 34. Katika Baadhi ya doria hizo kamati iliweza kukamata vifaa mbalimbali na mazao ya msitu. Kutokana na wahalifu waliokamatwa jumla ya shilingi 3,938,700 zilikusanywa kama faini na uuzaji wa mazao yaliyotaifishwa. Hela hizi kiasi cha shilingi 2,856,750 zimetumika kwa matumizi mbalimbali kama posho kwa wanakamati walioenda doria, asilimia 10 ya matumizi ya kijiji ambazo zimetumika kwa matumizi ya ofisi na miradi ya jamii, posho kwa watu waliotoa taarifa za kuwezesha kukamata waalifu. Hela nyingine (1,081,950) bado zimebaki kwenye mifuko ya kamati za maliasili.

Kamati za maliasili bado hazijafungua akaunti benki licha ya kuwa na uwezo wa kukusanya mapato ya faini na mapato mengine yatokanayo na matumizi endelevu ya mazao ya msitu.

### UPASHANAJI HABARI NA UHAMASISHAJI

Mradi umetumia magazeti na vyombo vya habari kutangaza mafanikio na changamoto za mradi. Kwa kipindi hiki Mradi umetumia Radio Abood na Clauds kutangaza habari mbalimbali kama mafunzo ya kilimo hifadhi, mafanikio ya vikundi vya hisa na uharibifu unaoendelea kwenye misitu ya Kanga na Mkingu.

Mradi ulitumia njia ya Mikutano na sinema kuelezea matarajio na shughuli za mradi. Pia kupitia sinema elimu juu ya UKIMWI ilitolewa kwa njia ya sinema na vipeperushi vilivyosambazwa wakati wa sinema. Kwenye zoezi hili jumla ya vijiji 28 vilifikiwa na makisio ya watu wasio pungua 1200. Pia vipeperushi 105 vinavyo husu ugonjwa wa UKIMWI vilisambazwa.




Mradi umechapisha fulana 200 zenye ujumbe wa utawala bora. Baadhi ya fulana zimeshasambazwa kwa viongozi wa kamati za maliasili na viongozi wa serikali ya kijiji.

## UHARIBIFU WA MSITU WA MAZINGIRA ASILIA YA MKINGU

Kutokana na ufuatiliaji uliofanywa na Shirika la kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG) wakishirikiana na Mradi wa AVA inaonesha kwamba kwa kipindi cha mwaka mmoja kuanzia Octoba 2014 hadi Septemba 2015 Msitu wa mazingira asilia ya Mkingu umeweza kupoteza hekta 90 ambayo ni sawa na 0.6% ya uharibifu wa msitu kwa mwaka.



*Shamba la maharage lililopo ndani ya Msitu wa Hifadhi ya Mazingira Asilia ya Mkingu*




KWA MAWASILIANO ZAIDI

Mkurugenzi Mtendaji TFCG: S.L.P 23410, Dar es Salaam,

Simu: +255 22 2669007,Barua pepe: tfcg@tfcg.or.tz/www.tfcg.org

Mkurugenzi Mtendaji MJUMITA: S.L.P 21522, Dar es Salaam,

Simu: +255 22 2669007Kwa wanajamii wa Wilaya ya Mvomero wanaweza kuwasiliana na Meneja wa mradi Ndugu Hassan Chikira Kwa namba zifuatazo:

Simu ya mkononi: 0782217846 au 0715546448